**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB), WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU) KATIKA MKUTANO WA UTEKELEZAJI WA SHERIA NA. 5 YA 2003 YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI TAREHE 21 SEPTEMBA, 2018**

- **Bw. Peter Kalonga; Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu: Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu,**
- **Bi Khadija Mwenda, Kaimu Mtedaji Mkuu wa OSHA,**
- **Ndugu, Wakurugenzi wa Sera na Mipango na Wakurugenzi wa Utawala na Raslimaliwatu kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali,**
- **Ndugu, Wakurugenzi na Maofisa toka Ofisi ya Waziri Mkuu**
- **Ndugu, Watalaam na Wafanyakazi wa OSHA,**
- **Ndugu, Waandishi wa Habari kutoka katika vyombo Mbalimbali,**
- **Mabibi na Mabwana,**

Tumsifu Yesu Kristu,
Bwaba Asifiwe,
Assalaam Aleykum.
Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia sote kuwa na afya njema iliyotuwezesha kufika hapa leo kwa ajili ya kushiriki mjadala wa pamoja na kupata maoni yenu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi Na. 5 ya mwaka 2003. Pia napenda kuwashukuru wote mliopokea mwaliko wetu na kuhudhuria katika semina hii kwani inaonesha ni jinsi gani mnavyolipa umuhimu suala zima la usalama sehemu za kazi.

Aidha, ninamshukuru Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA kwa maelezo ya utangulizi na kwa kunikaribisha katika kufungua semina hii ambayo ni ya muhimu sana kwa mustakabali wa uboreshaji wa mazingira ya afya na usalama mahali pa kazi, sio tu katika Sekta Binafsi bali pia katika Sekta ya Umma. Mimi binafsi nimefurahi kupata fursa hii ya pekee ili kufungua semina hii ambayo ni ya kwanza na ya aina yake hasa kwa Watendaji wa ngazi ya juu ndani ya Wizara na Mashirika ya Umma.

Katika semina hii mtaweza kuwasikiliza wataalam wetu watakaochokoza mada mbalimbali. Nimeambiwa kuwa baadhi ya mambo mtakayozungumuza ni pamoja na Utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama mahala pa kazi pamoja na kanuni zake, Majukumu ya wakala wa OSHA, umuhimu wa kuwa na sehemu ya kazi inayozingatia Afya na Usalama, Vihatarishi katika maofisi ambako ndiko wengi wetu tunakofanyia kazi na kukaa muda mrefu. Mfano wengi wetu tunakalia viti ambavyo havifai kwa afya zetu

ambavyo vinaweza kuleta maumivu ya mifupa kama sehemu za shingo, mgongo, mikono au kiuno n.k.

**Ndugu washiriki,**
Suala la kufanya kazi katika sehemu ambayo ina usalama na ni nzuri kiafya ni jambo ambalo lipo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake; Ibara ya 11(1) inazitaka Mamlaka za Nchi kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa maradhi au hali ya ulemavu, na katika hali nyinginezo. Katika kuhakikisha kuwa jambo hili linatekelezeka Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Afya na Usalama Mahala pa kazi ya Mwaka 2010 na kutunga Sheria ya Afya na Usalama mahala pa kazi Na.5 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2001 na Sheria ya Fidia kwa wafanyakazi Na. 20 ya mwaka 2008. Sheria hizi zimeunda vyombo vinavyohusika na kutoa elimu kwa ajili ya kuzuia ajali na kuhakikisha mahali pa kazi panakuwa salama na kuweza kumsaidia mfanyakazi kurudi kwenye hali yake anapopata matatizo akiwa kazini.

Haya yote yalilenga kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Na. 155 wa mwaka 1981, ambayo Tanzania ni mwanachama.

**Ndugu Washiriki**
Kama mnavyoelewa Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasisitiza suala la ujenzi wa Uchumi wa Viwanda ili kufikia malengo tuliyojiwekea kama Nchi kuwa ifikapo mwaka 2025 tuwe tumefikia kuwa nchi ya kipato cha kati.

Utekelezaji wa malengo haya unakwenda sambamba na suala la kuimarisha Usalama na Afya mahala pa kazi. Pia tunalenga kutekeleza malengo ya milenia hasa Lengo namba Nane (8) la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo ni kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wote ifikapo mwaka 2030.

**Ndugu Washiriki**
Juhudi hizi zote zinalenga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015, ibara ya 173 kifungu kidogo cha (b) ambacho kinaielekeza Serikali kuweka mikakati mbalimbali ili kuendelea kulinda afya na usalama wa wafanyakazi mahala pa kazi na kuondoa vihatarishi sehemu za kazi. Maagizo ya Mhe. Rais aliyoyatoa katika vipindi tofauti alipokutana na Wafanyabiashara na Wadau wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma.

**Ndugu Washiriki**
Katika kutekeleza maagizo ya Ilani ya Uchaguzi na Maagizo ya Viongozi wetu, Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa kazi (OSHA) umekuja na mkakati mpya wa kufanya mabadiliko ili kuweza kutoa huduma nzuri kwa Sekta ya Umma na sekta binafsi. Mikakati hiyo ni pamoja na

- Kutengeneza program maalum ya utoaji Elimu kwa wadau kuhusu takwa la kisheria la kulinda afya za wafanyakazi nchini mahala pa kazi katika Kanda mbalimbali

- Kusimamia mifumo ya utendaji wa watumishi wa OSHA ili kuondoa mianya ya rushwa na kukuza uzalendo na uwajibikaji.

- Kuondoa baadhi ya Ada na tozo zisizoondoa wajibu wa muajiri kulinda Afya za Wafanyakazi mbali zinazoondoa mzigo wa mwekezaji katika kuwekeza kwenye uchumi hasa uchumi wa viwanda.

**Tozo zilizoondolewa au kufanyiwa marekebisho ni pamoja na:-**

| **Na** | | **Mwanzo** | **Sasa** | **Sababu** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kufuta ada ya Fomu ya Usajili | Tsh. 2,000 | Imefutwa | Kupunguza gharama. |
| 2. | Kufuta ada ya Usajili wa maeneo ya kazi kwa kuzingatia ukubwa wa eneo. | (iliyokuwa ikitozwa Tshs 50,000 hadi Tshs 1,800,000 kulingana na eneo la kazi), | Imefutwa. | Kuboresha mazingira ya biashara. |
| 3. | Kufuta faini inayohusiana na vifaa vya kuzimia moto | Tshs. 500,000 | Imefutwa Kuondoa *Double payment* | Kupunguza gharama za uendeshaji. |
| 4. | Kufuta ada ya Leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi | iliyokuwa ikitozwa Tshs 200,000 kwa mwaka) | Imefutwa | Kuboresha mazingira ya biashara. |
| 5. | Kufuta Tozo ya siku ya Ushauri wa kitaalamu wa Usalama na Afya kwa kuzingatia idadi ya wafanyakazi. | Tshs 450,000 | Imefutwa | Kupunguza gharama ili kutoa elimu kwa wahitaji wengi zaidi. |

- Kutoa mafunzo kwa wataalam wetu kutokana na kubadilika kwa Teknolojia ya wawekezaji kuja na teknolojia ambayo inaweza kuzalisha viatarishi ambavyo ni vipya.

**Ndugu Washiriki,**
Kama mnavyotambua kwa sasa nchi yetu kwa sasa inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Miradi hiyo ni kama Ujenzi wa Madaraja ya Juu, upanuzi wa viwanja vya ndege mfano uwanja wa kimataifa Julius Nyerere, ujenzi wa reli ya kisasa (standard gauge), miradi mikubwa ya umeme, mradi mkubwa wa bomba la mafuta, na miradi mingine mingi mikubwa ambayo Serikali ya awamu tano inaendelea kutekeleza. Katika miradi yote hii OSHA imekuwa ikisimamia na inaendelea kusimamia Usalama na Afya

kwa wafanyakazi wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo. Matokeo ya usimamizi huu ni kwamba umepelekea kupunguza ajali na magonjwa, migogoro kazini, kupunguza gharama za utekelezaji na hivyo kufanya miradi hiyo kukamilika katika viwango vilivyokusudiwa na kumalizika kwa wakati.

**Ndugu washiriki**

Kazi nzuri inayoendelea kufanywa na OSHA ya kutoa elimu ili kuzuia ajali imeendelea kuwa na matokeo mazuri. Mfano, kwa mwaka wa fedha 2017/18 imesaidia kupunguza ajali ambapo jumla ya ajali 755 ziliripotiwa kwa mujibu wa Sheria, ambapo 6 kati ya hizo zilisababisha vifo, 749 majeruhi. Aidha, Sekta ya Uzalishaji iliongoza kwa kuwa na asilimia 87 ya ajali zote ambapo sekta ya madini ilikuwa na asilimia 7, ujenzi asilimia 4 Sekta zilizobaki asilimia 2.

Katika Takwimu hizi utaona kama Sekta ya Umma haikuguswa sana lakini bado kuna umuhimu wa kuwa na elimu itusaidie kuzuia na kutoa taarifa pindi zinapotokea ajali. Hivyo basi mnaona ni kwa namna gani ni muhimu kwa wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kuwa na uelewa wa namna ya kuripoti taarifa hizo, ili zisaidie katika kutengeneza sera na miongozo mbalimbali ya kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi, na hivyo kuleta uzalishaji endelevu na wenye tija.

**Ndugu Washiriki**
Kutokana na msingi huo wakala unatilia mkazo wa elimu kwa Sekta ya Umma ikizingatiwa kuwa miradi hii mikubwa inajengwa kwa ushirikiano wa wataalam toka sekta ya Binafsi na wataalam na wasimamizi wakuu toka sekta ya Umma hivyo ni vizuri kujua vihatarishi na kuchukua hatua.

**Ndugu washiriki**,
Uboreshaji wa masuala ya afya na usalama kazini ni jukumu la Waajiri na Wafanyakazi wote. Waajiri kwa kushirikiana na Wafanya kazi wanapaswa kuweka mikakati ya kuvitambua na kuviondoa vihatarishi sehemu zao za kazi ili kuzuia madhara yanayoweza kuwapata wafanyakazi wakiwa kazini. Mikakati hiyo inapaswa kufuata miongozo yote inayotolewa na Taasisi ya OSHA.

**Ndugu washiriki**,
napenda niwakumbushe kuwa sehemu zetu za kazi katika Sekta ya Umma ni sehemu kama zilivyo sehemu za kazi katika Sekta Binafsi japokuwa mazingira ya ufanyaji kazi yanaweza kuwa tofauti. Kwa hiyo lengo la semina hii ya leo ni kutaka kutoa elimu kwenu nyinyi viongozi waandamizi wa Wizara na Mashirika yetu kwamba na sisi ndani ya Sekta ya Umma tunapaswa kutekeleza sheria hii kama walivyo waajiri wengine katika Sekta Binafsi. Kwa muda mrefu hii Sheria imekuwa ikitekelezwa zaidi kwenye Sekta Binafsi. Ni ukweli uliowazi kuwa ndani ya Serikali na katika maofisi yetu tunakabiliwa na vihatarishi vya afya na usalama wetu kama ilivyo katika sekta binafsi. Japokuwa aina ya vihatarishi inaweza kuwa tofauti. Naomba nitoe wito kwenu katika mambo yafuatayo:

1. Katika kila ofisi zetu za Umma nasi tufanye tathmini ya vihatarishi *(Risk Assessment)* ili itusaidie kuboresha mazingira yetu ya kazi.

2. Wafanyakazi wapatiwe mafunzo ya afya na usalama kazini ili wawe na uwezo wa kutambua vihatarishi sehemu zao za kazi na namna ya kujilinda na vihatarishi hivyo.

3. Wafanyakazi wapimwe afya zao ili kusaidia kuwa na nguvu kazi iliyo imara

Hivyo ili kufanikisha hayo OSHA itaendelea kutoa elimu maeneo yetu ya kazi ili tuweze kutekeleza matakwa ya Sheria na kusimamia kwa ukamilifu namna bora ya utekelezaji kwa watu tunaowasimamia.

**Ndugu Washiriki,**
Nikamilishe kwa kuwakumbusha kwamba semina hii ni muhimu sana hivyo niwaombe tena mjadili na kutoa maoni yatakayotusaidia kuboresha ikizingatiwa kuwa maazimio mtakayatoka nayo yatafanikisha nia ya Serikali ya kuweka mazingira salama ya kufanyia kazi kwa watumishi wetu. Baada ya kusema maneno haya, ninawatakia semina njema na

**NINATAMKA KUWA SEMINA HII IMEFUNGULIWA RASMI.**

**ASANTENI SANA**